

KUMB: PPR/17 - 07/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMAMOSI, TAREHE 1 JULAI 2017**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumamosi, Tarehe 1 Julai 2017**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Juni 2017. Kwa mwezi Julai 2017, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa TZS 37/lita sawa na asilimia 1.81, TZS 14/lita sawa na asilimia 0.73, na TZS 19/lita sawa na asilimia 1.03, sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa nazo zimepungua kwa TZS 37.21/lita sawa na asilimia 1.92, TZS 13.70/lita sawa na asilimia 0.77, na TZS 18.85/lita sawa na asilimia 1.10, sawia. Pamoja na ongezeko la ushuru wa bidhaa za mafuta ya petroli la TZS 40/lita kuanzia mwezi Julai 2017, bei za mafuta kwenye soko la ndani zimepungua, kwa kiasi kikubwa kupungua huku kumetokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji mafuta hayo (*BPS premiums*).
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli zimeongezeka katika mkoa wa Tanga ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Juni 2017. Kwa mwezi Julai 2017, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa TZS 43/lita sawa na asilimia 2.19 na TZS 4/lita, sawa na asilimia 0.21, sawia. Aidha, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Tanga nazo zimepungua kwa TZS 43.07/lita sawa na asilimia 2.33 na TZS 3.81/lita sawa na asilimia 0.22, sawia. Ongezeko la bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa Tanga linatokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia kwa mzigo mpya uliopokelewa katika bandari ya Tanga mwezi Juni 2017 ukilinganisha na bei ya mzigo wa mwisho kupokelewa katika bandari hiyo mwezi Aprili 2017. Kutokana na kutokupokea mzigo mpya wa Mafuta ya Taa katika bandari ya Tanga kwa mwezi Juni 2017, Wamiliki wa Vituo vya Mafuta mkoa wa Tanga wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam. Hivyo, bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mkoa wa Tanga zitatokana na gharama za mafuta hayo yaliyopokelewa kwenye bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa hadi Tanga.
- (c) Ni vizuri ikumbukwe ya kwamba, katika Bunge la Bajeti linaloendelea Dodoma, Bunge lilipitisha Muswada wa mabadiliko ya Ushuru wa Bidhaa za mafuta ya petroli yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa ambapo Shilingi 40 kwa kila lita moja ya mafuta hayo zimeongezwa kwenye viwango vya awali vya Ushuru wa Bidhaa uliokuwa unatozwa. Muswada umeainisha ya kwamba, ongezeko hilo la Shilingi 40 kwa lita litekelezwe kuanzia tarehe 1 Julai, 2017. Kwa kuzingatia muswada huo uliopitishwa na Bunge bajeti, katika ukokotoaji wa bei za mafuta ya petroli kwa mwezi Julai, 2017, EWURA imeongeza gharama ya Shilingi 40 kwa lita moja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa.

- (a) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana vile vile kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo ziwe chini ya bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017.****
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (e) Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,014	1,874	1,806
Arusha	2,098	1,958	1,890
Arumeru (Usa West)	2,098	1,958	1,890
Karatu	2,117	1,976	1,908
Monduli	2,104	1,963	1,895
Monduli-Makuyuni	2,108	1,968	1,900
Ngorongoro (Loliondo)	2,190	2,049	1,981
Kibaha	2,019	1,879	1,810
Bagamoyo	2,025	1,885	1,817
Kisarawe	2,021	1,881	1,813
Mkuranga	2,024	1,884	1,815
Rufiji	2,042	1,902	1,833
Dodoma	2,073	1,933	1,864
Bahi	2,080	1,940	1,872
Chemba	2,099	1,959	1,891
Kondoa	2,106	1,965	1,897
Kongwa	2,070	1,930	1,862
Mpwapwa	2,074	1,934	1,865
Iringa	2,078	1,938	1,870
Kilolo	2,083	1,942	1,874
Mufindi (Mafinga)	2,088	1,948	1,880
Njombe	2,106	1,966	1,898
Ludewa	2,144	2,004	1,936
Makete	2,137	1,997	1,929
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,104	1,964	1,896
Bukoba	2,229	2,089	2,021
Biharamulo	2,204	2,063	1,995
Karagwe (Kayanga)	2,246	2,105	2,037
Kyerwa (Ruberwa)	2,251	2,111	2,043
Muleba	2,229	2,089	2,021
Ngara	2,195	2,054	1,986
Misenyi	2,238	2,097	2,029
Geita	2,179	2,039	1,971
Bukombe	2,168	2,028	1,960
Chato	2,200	2,060	1,992
Mbogwe	2,217	2,077	2,009
Nyang'hwale	2,194	2,054	1,986
Kigoma	2,245	2,105	2,037
Uvinza (Lugufu)	2,257	2,117	2,049

Buhigwe	2,234	2,094	2,026
Kakonko	2,202	2,062	1,994
Kasulu	2,231	2,091	2,023
Kibondo	2,209	2,069	2,001
Moshi	2,088	1,948	1,879
Hai (Bomang'ombe)	2,091	1,951	1,882
Mwanga	2,081	1,941	1,872
Rombo (Mkuu)	2,109	1,968	1,900
Same	2,074	1,934	1,866
Siha (Sanya Juu)	2,094	1,954	1,886
Lindi	2,073	1,933	1,864
Lindi-Mtama	2,091	1,951	1,882
Kilwa Masoko	2,048	1,908	1,839
Liwale	2,094	1,954	1,885
Nachingwea	2,102	1,962	1,894
Ruangwa	2,104	1,964	1,895
Babati	2,136	1,996	1,928
Hanang (Katesh)	2,147	2,007	1,938
Kiteto (Kibaya)	2,147	2,007	1,939
Mbulu	2,149	2,009	1,941
Simanjiro (Orkasumet)	2,168	2,028	1,960
Musoma	2,192	2,052	1,984
Musoma Vijijini (Busekela)	2,233	2,093	2,024
Rorya (Ingirijuu)	2,201	2,061	1,993
Rorya (Shirati)	2,236	2,096	2,027
Bunda	2,184	2,043	1,975
Butiama	2,189	2,049	1,981
Serengeti (Mugumu)	2,238	2,098	2,029
Tarime	2,203	2,063	1,995
Mbeya	2,121	1,981	1,913
Chunya	2,131	1,990	1,922
Chunya (Makongolosi)	2,145	2,004	1,936
Ileje	2,134	1,994	1,926
Kyela	2,137	1,997	1,928
Mbarali (Rujewa)	2,105	1,965	1,897
Mbozi (Vwawa)	2,130	1,990	1,922
Momba (Chitete)	2,139	1,999	1,931
Rungwe (Tukuyu)	2,130	1,990	1,921
Morogoro	2,039	1,899	1,831
Mikumi	2,055	1,915	1,846
Kilombero (Ifakara)	2,077	1,937	1,868
Kilombero (Mlimba)	2,099	1,959	1,891
Kilombero (Mngeta)	2,089	1,948	1,880
Ulanga (Mahenge)	2,088	1,947	1,879
Malinyi	2,098	1,958	1,889

Kilosa	2,058	1,917	1,849
Gairo	2,058	1,917	1,849
Mvomero (Wami Sokoine)	2,050	1,909	1,841
Turian	2,064	1,924	1,856
Mtwara	2,087	1,946	1,878
Nanyumbu (Mangaka)	2,135	1,995	1,927
Masasi	2,112	1,972	1,904
Newala	2,119	1,978	1,910
Tandahimba	2,112	1,971	1,903
Mwanza	2,164	2,024	1,955
Kwimba	2,200	2,060	1,992
Magu	2,172	2,032	1,963
Misungwi	2,170	2,029	1,961
Sengerema	2,196	2,056	1,988
Ukerewe	2,223	2,083	2,015
Sumbawanga	2,187	2,046	1,978
Kalambo (Matai)	2,179	2,039	1,971
Nkasi (Namanye)	2,200	2,060	1,992
Katavi (Mpanda)	2,222	2,081	2,013
Mlele (Inyonga)	2,200	2,060	1,992
Songea	2,137	1,997	1,929
Mbinga	2,171	2,031	1,962
Namtumbo	2,167	2,026	1,958
Nyasa (Mbamba Bay)	2,173	2,033	1,965
Tunduru	2,196	2,056	1,988
Shinyanga	2,143	2,003	1,934
Kahama	2,157	2,016	1,948
Kishapu	2,171	2,031	1,963
Simiyu (Bariadi)	2,184	2,044	1,976
Busega (Nyashimo)	2,177	2,037	1,969
Itilima (Lagangabilili)	2,187	2,047	1,979
Maswa	2,176	2,035	1,967
Meatu (Mwanhuji)	2,183	2,042	1,974
Singida	2,105	1,964	1,896
Iramba	2,117	1,977	1,908
Manyoni	2,089	1,949	1,881
Ikungi	2,100	1,960	1,892
Mkalama (Nduguti)	2,129	1,989	1,921
Tabora	2,168	2,028	1,960
Igunga	2,122	1,982	1,914
Kaliua	2,186	2,046	1,978
Ulyankulu	2,180	2,040	1,972
Nzega	2,133	1,992	1,924
Sikonge	2,180	2,040	1,971
Urambo	2,181	2,041	1,973

Tanga	2,006	1,862	1,852
Handeni	2,026	1,883	1,831
Kilindi	2,041	1,898	1,866
Korogwe	2,018	1,874	1,845
Lushoto	2,027	1,884	1,854
Mkinga (Maramba)	2,013	1,869	1,866
Muheza	2,010	1,867	1,852
Pangani	2,012	1,869	1,858

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,903.33	1,762.98	1,694.66

Bei za Jumla-TANGA	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)
Bei Kikomo	1,894.68	1,751.09

Eng. Godwin Samwel

**KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA**